

MWALO NA SOKO LA SAMAKI - KIBIRIZI (KIGOMA)

Mradi wa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji (LIC) ni mradi wa kuendeleza sekta binafsi unaofadhiliwa na Danida. Mradi unashughulikia vikwazo vikuu vinavyokwamisha maendeleo ya biashara na ukuaji wa uchumi katika ngazi ya wilaya kwenye mikoa miwili ya Dodoma na Kigoma nchini Tanzania. LIC imejikita katika mijadala kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, miundombinu ya utoaji wa huduma za biashara ikiwa ni pamoja na vituo vya pamoja vya biashara na miundombinu ya pamoja kati ya sekta ya umma na sekta binafsi ili kusaidia maendeleo ya biashara na uwekezaji. Washirika wanaotekeleza mradi wa LIC ni Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Sekretariati za mikoa ya Kigoma na Dodoma, Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) Tanzania, Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT), Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Chemba ya Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA).

Kwa mwaka 2016, mradi wa LIC kwa kuitikia wito kutoka Manispaa ya Kigoma Ujiji ulianzisha uwekezaji ili kuboresha mwalo na soko la samaki la Kibirizi. Uboreshaji wa miundombinu ulijumuisha kuweka sakafu mpya ya vigae (pavements) kwenye eneo la mwalo, mitaro, maduka, mifumo ya maji safi na maji taka, uwekaji wa umeme, sehemu za kukaushia/kuanikia dagaa, vyumba maalum na vifaa vya kuhifadhi samaki na kwa mara ya kwanza uzalishaji wa barafu mkoani humo. Katika kusaidia uwekezaji huu, mfumo mpya wa uongozi uliundwa kupitia Special Purpose Vehicle (SPV).



Sehemu mpya ya kukaushia dagaa




Mkusanya mapato akiwa na mashine mpya za kukusanyia mapato

Dhana ya SPV

Kutambua changamoto katika kusimamia mwalo wenye shughuli nyingi za kibiashara kama soko la samaki la Kibirizi, KUMC pamoja na LIC waliamua kupitisha usimamizi wa soko kwa kampuni kwa ubia wa pamoja kati ya sekta binafsi na serikali (PPP) unaojulikana kama SPV chini ya jina la Kibirizi Landing Site Company Limited (KLSC). Kampuni hii mpya imesajiliwa kikamilifu kama kampuni yenye ukomo wa dhama na imeanza shughuli zake tarehe 6 Agosti mwaka 2018. Kampuni ina bodi yake binafsi, uongozi/menejimenti na wafanyakazi. KUMC wanabaki kuwa wamiliki wa mali na wanapokea mapato kufuatana na makubaliano na kampuni ya SPV. Kampuni inawajibika kwa shughuli zote, matengenezo na kusimamia uwekezaji mpya wa Kibirizi ikifuata muongozo wa bodi ya Kampuni. Watumiaji (wavuvi, wafanyabiashara wanawake na wanaume na makampuni ya uvuvi) kwenye Mwalo na soko la samaki wanawakilishwa kwenye bodi kupitia vyama vyao pamoja na KUMC and LIC.



Wanawake wakiuza dagaa kwenye mwalo wa samaki (ufukwe wapanapovuliwa samaki)



Sakafu mpya iliyojengwa na majengo ya ofisi yaliyokarabatiwa yanayotumiwa na KLSCL

Maboresho, mambo muhimu na matarajio

- Mwalo unategemea kuhudumia boti za samaki 400 na kutengeneza faida ya milioni 80 katika mwaka wa kwanza wa kufanya kazi.
- Kupitia upatikanaji wa mabonge ya barafu na chengachenga za barafu, vyumba maalum vya baridi vya kuhifadhia samaki na mazingira bora ya kufanyia biashara, wavuvi wanatarajiwa kupunguza hasara ya baada ya mavuno kutoka 35% mpaka 10% na kuongeza kipato kwa 30%. Kupunguza hasara baada ya mavuno kutafanikiwa kwa kutumia barafu katika mashua/boti, masokoni, wakati wa usafirishaji na kupitia mafunzo ya kuongeza ufahamu juu ya kuboresha usafi na utunzaji wa samaki. Upatikanaji wa barafu umewezesha kusafirisha samaki nje ya mkoa mfano mkoa wa Tabora.
- Kuongezeka biashara ya dagaa na samaki wenye ubora unatarajiwa kutengeneza kwa kiwango cha chini cha ajira mpya 130 na athari chanya kubwa katika usafiri, biashara, pembejeo na biashara za kuongeza thamani za mazao inatarajiwa kuwa shilingi milioni 280 kwa mwaka wa kwanza.
- Uchumi unaweza kukua mara mbili zaidi kama mwalo huu wa samaki la Kibirizi utakuwa mwalo rasmi na kufunga mialo yote ambayo sio rasmi jirani na mwalo wa Kibirizi. Hilo litawezekana iwapo viwango vitaboreshwa na huduma zipatikanazo Kibirizi zitaongezeka
- Kuboresha miundombinu na huduma kwa wasafirishaji samaki kwenda nje ya nchi kunatarajiwa kupelekea ongezeko katika ubora wa bidhaa zinazosafirishwa na kukidhi viwango usafi vya kimataifa
- Mpango wa awamu ya pili utaboresha miundombinu katika soko la samaki na kuongeza uwezo wa kukausha dagaa
- Kwa kushirikiana na wawakilishi wa wavuvi, KUMC na LIC wataendelea kutafuta fursa za kuboresha huduma na masoko ya samaki na bidhaa za samaki
- Wawekezaji wapya wa binafsi katika usindikaji na uuzaji wanatarajiwa kunufaika na vifaa bora katika soko la Kibirizi.

Kwa taarifa zaidi, tafadhali tembelea tovuti ya mradi wa LIC: www.lic.or.tz

Septemba 2018